



UCHAMBUZI KUHUSU HALI YA UWAJIBIKAJI, UWAZI NA RUSHWA KATIKA SEKTA ZA ELIMU NA AFYA TANZANIA

1.0 UTANGULIZI

TYVA ni Asasi ya vijana isiyo na malengo yoyote ya kisiasa, Ilianzishwa mwaka 2000 na kusajiliwa chini ya Wizara ya mambo ya ndani Julai 28, 2002 kama asasi ya kiraia kwa namba (S.O NO 11454) kufanya kazi ya kuwajengea uwezo vijana nchini.

TYVA ina dhamira ya kufanya ushawishi na utetezi wa kundi la vijana kuhusu kuishauri Serikali kufanya maboresho mapana ya sekta za elimu na afya. Hivyo kabla ya kufikia hatua hiyo TYVA imekusudia kupata uelewa mpana wa hali ilivyo katika uwajibikaji, Uwazi na rushwa katika sekta za Elimu na Afya.

Ili kufikia dhamira yake, TYVA iliunda kikosi kazi cha wanachama[1] wake watano wakiongozwa na mtaalamu[2] mwelekezi (Consultant) ilifanya uchambuzi kupitia rejea mbalimbali (desktop review) yaliyoorodheshwa katika sehemu ya mwisho ya nyaraka hii yanayohusu rushwa, uwajibikaji, Uwazi na rejea kuhusu muktadha wa sekta ya elimu na afya.

Uchambuzi huu umegawanyika katika maeneo makuu manne, mosi ni utangulizi wa uchambuzi, pili ni hali ya uwajibikaji na Uwazi katika sekta za elimu na afya, tatu ni hali ya rushwa katika sekta za elimu na afya na nne ni hitimisho la uchambuzi.

Kwa ufupi hali ya uwajibikaji na Uwazi katika sekta za elimu na afya imeainisha muktadha (context) ya sekta hizo kwa ufupi na namna zinavyoratibiwa na mifumo ya utawala. Pia sehemu hii imechambua dhana ya uwajibikaji kama ilivyobainishwa kwa mujibu wa Ibara ya 8 ibara ndogo ya (1) aya (c) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuwa wananchi ndio msingi wa madaraka ya Serikali na kuwa kuwa Serikali itawajibika kwa wananchi. Kwa kuzingatia muktadha na dhana ya uwajibikaji, uchambuzi huu ulizichambua hoja tano (5) za uwajibikaji kwenye sekta ya elimu na hoja 5 kwenye sekta ya afya. Hoja hizo za uwajibikaji ni kama zilivyoripotiwa mdhabiti mkuu na mkaguzi wa hesabu za Serikali katika hesabu za Jumla za Serikali Kuu na hesabu za Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2016/17.

Kwenye sehemu ya tatu, uchambuzi wa hali ya rushwa sekta za elimu na afya, uchambuzi umezungumzia maana ya rushwa na msingi uliotumiwa. Katika eneo hili uchambuzi umetoa hali halisi juu ya mitazamo mitatu ya Watanzania juu ya rushwa na mwishoni ni hali ya rushwa ilivyo kwenye sekta za elimu na afya.

2.0 HALI YA UWAJIBIKAJI NA UWAZI SEKTA ZA ELIMU NA AFYA

2.1 Sekta za Elimu na Afya kwa ufupi

Sekta ya Elimu nchini Tanzania inaongozwa na sera ya elimu ya mwaka 2014 inayosimamiwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Sera hii inaweka bayana dira yake kwa ni “Kuwa na Mtanzania aliyeelimika na mwenye maarifa, stadi, umahiri, uwezo na mitazamo chanya ili kuweza kuchangia katika kuleta maendeleo ya Taifa.”

Kwa upande wa pili, Sekta ya afya nchini Tanzania inaongozwa na sera ya afya ya mwaka 2007 inayosimamiwa na wizara ya afya, maendeleo ya jamii, jinsia, wazee na watoto. Dira ya Sera hii inataka kuona tuna “kuwa na jamii yenye afya bora na ustawi ambayo itachangia kikamilifu katika maendeleo binafsi na ya nchi”.

Mfumo wa utawala nchini umeruhusu matumizi ya fedha za umma kwenye sekta ya elimu na sekta ya afya kufanywa baina ya wizara husika pamoja na uratibu wa maendeleo ngazi za chini katika maeneo walipo wananchi chini ya wizara ya OR-TAMISEMI (Ofisi ya Rais- Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.) Wizara ya OR-TAMISEMI inaratibu utoaji wa wa elimu katika ngazi zote za elimu ya Awali, Msingi hadi Sekondari; wakati huo huo Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inasimamia elimu ya juu na vyuo vyote vya ufundi.

Katika kipindi cha kuanzia Julai 2017 hadi Februari, 2018 Serikali imeripoti kutoa jumla ya shilingi bilioni 172.4 kugharamia Mpango wa Elimu msingi bila Malipo ambapo kati ya hizo shilingi bilioni 77.2 zimetolewa kwa shule za msingi na shilingi bilioni 89.2 zilitolewa kwa shule za sekondari nchini. Wanafunzi waliohitimu Darasa la Saba Mwaka 2017 walikuwa 909,950, wakiwemo wasichana 480,784 na wavulana 429,166. Kati ya hao, wanafunzi 662,035 wakiwemo wasichana 341,020 na wavulana 321,015 walifaulu mtihani huo sawa na asilimia 72.75. Kwa upande wa Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Nne, jumla ya wanafunzi 287,713 (wasichana 143,728 na wavulana 143,985) walifaulu mtihani huo katika Mwaka 2017 sawa na asilimia 77.09 ikilinganishwa na wanafunzi 374,950 (wasichana 191,956 na wavulana 182,994) waliofanya Mtihani huo. Ufaulu katika Mtihani wa Kidato cha Nne umeongezeka kutoka asilimia 75.99 Mwaka 2016 hadi asilimia 77.09 kwa Mwaka 2017. Kati ya wanafunzi 62,725 waliofanya mtihani wa Kidato cha Sita Mwaka 2017, wanafunzi 61,308 walifaulu sawa na asilimia 97.74 ikilinganishwa na wanafunzi 63,525 waliofaulu Mwaka 2016. (Hotuba ya Bajeti: OR-TAMISEMI, 2018/2019).

Hospitali za rufaa za mikoa zenyewe zipo chini ya uratibu wa Wizara ya Afya. Katika kipindi cha Julai 2017 hadi Machi 2018, Hospitali za Rufaa za Mikoa (28) zilihudumia jumla ya wagonjwa 1,637,835 ambapo wagonjwa wa nje walikuwa 1,329,364 na wagonjwa wa ndani walikuwa 308,471 (Hotuba ya Bajeti: Wizara ya Afya, 2018/19). Aidha wizara ya afya, maendeleo ya jamii, jinsia, wazee na watoto inasimamia pia wakala na tasisi za kiafya kama, Bohari ya Dawa ya serikali, Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu, Wakala wa Maabara ya Mkemia wa Serikali, Mamlaka ya Chakula na Dawa, Taasisi ya Chakula na Lishe, Taasisi ya Saratani ya Ocean Road, Taasisi ya Mifupa MOI na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya.

Wakati Wizara ya Afya ikifanya hivyo kwa upande wa pili, OR- TAMISEMI inahusika na uratibu pamoja na usimamizi wa Hospitali za Halmashauri, Vituo vya Afya na Zahanati ili kuhakikisha zinatoa huduma bora za afya kwa wananchi. Hospitali za Halmashauri zilizopo ni 120 kati ya Hospitali 184 zinazohitajika sawa na asilimia 65 ya lengo. Kati ya Hospitali hizo, 77 zinamilikiwa na Serikali na 43 zinamilikiwa na Mashirika Binafsi ambazo ni Hospitali Teule zilizoingia mkataba wa utoaji huduma na Halmashauri. Vituo vya Afya vilivyopo ni 696 sawa na asilimia 15.7 ya lengo la kuwa na Vituo vya Afya 4,420. Kati ya hivyo, vituo 513 vinamilikiwa na Serikali na vituo 183 vinamilikiwa na Sekta Binafsi na Mashirika ya Dini. Idadi ya Zahanati zilizopo nchini ni 6,640 sawa na asilimia 53 ya lengo la kuwa na Zahanati 12,545 zinazohitajika. Kati ya hizo, zahanati 4,554 sawa na asilimia 47.9 zinamilikiwa na Serikali na Zahanati 2,086 zinamilikiwa na Sekta Binafsi. (Hotuba ya Bajeti: OR-TAMISEMI, 2018/2019).

Kwenye Hotuba ya Bajeti, OR-TAMISEMI mwaka wa fedha 2018/19 iliripotiwa kuwa kuna wanachama 12,278,406 waliojiunga na na Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) mpaka kufikia mwaka 2017. Imeelezwa kuwa wananchi katika Halmashauri 154 kati ya 185, wanatumia kadi za CHF na TIKA katika maeneo ya miji. Imeelezwa kuwa Halmashauri zimetunga Sheria Ndogo ambazo zimeweka viwango vya kuchangia kati ya shilingi 5,000 hadi 30,000 kwa kila mwanachama ambapo fedha zilizokusanywa zimefikia bilioni 22 hadi kufikia mwezi Machi, 2018. Wakati huo huo idadi ya akinamama wanaojifungulia katika vituo vya kutolea huduma inaendelea kuongezeka hadi kufikia asilimia 68.5 mwezi Februari 2018 katoka asilimia 64 mwaka 2015/16. (Hotuba ya Bajeti: Wizara ya Afya, 2018/19)

2.2 Dhana Uwajibikaji – Sekta ya Elimu na Afya

Kwa mujibu wa Ibara ya 8 ibara ndogo ya (1) aya (c) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imetamkwa bayana kuwa Serikali itawajibika kwa wananchi. Kwa kuwa wananchi huichagua Serikali katika dhana ya uwakilishi hali kadhalika huwachagua wabunge kuwasaidia kuiwajibisha Serikali. Hivyo basi, “Uwajibikaji ni hali ya kiongozi na mtendaji kuwa tayari kujibu, kubeba dhamana na kutoa maelezo kwa wananchi juu ya maamuzi au matendo aliyoyafanya katika kutekeleza dhamana aliyopewa” (Policy Forum: Mwongozo wa Utawala Bora, 2013)

Kwa kuwa Serikali hukusanya kodi kwa ajili ya kutimiza lengo kuu la ustawi wa wananchi kwa mujibu wa ibara ya 8 ibara ndogo ya (1) aya (d); Fedha zinazokusanywa ni fedha za umma, hivyo dhana ya uwajibikaji na uwazi kwenye sekta ya elimu na afya inazileta pamoja Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, watoto na wazee pamoja na na OR-TAMISEMI na kutakiwa kuwajibika kwa wananchi kupitia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kamati za kudumu za Bunge zinazoshughulikia uwajibikaji wa Serikali Kuu (Kamati ya Ukaguzi wa Hesabu za Mashirika ya Umma - PAC) na Kamati ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali za Mitaa - LAAC) hupitia ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kuzichambua na kutoa mapendekezo yake kwa Bunge zima ili Bunge liwajibishe Serikali katika eneo la matumizi ya fedha za umma katika kufikisha huduma kwa wananchi.

Katika uchambuzi huu, tumepitia ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) za Serikali kuu na Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2016/2017 tukijikita katika kuangalia namna CAG alivyoibua hoja mbalimbali za ukaguzi kwenye sekta ya Elimu na Afya huku tukihitimisha maoni yetu kuhusu namna hoja hizo zinavyoathiri vijana wa jinsia zote za wanawake na wanaume. Hoja hizo bado zinaendelea pia kuchambuliwa na Kamati za Kudumu za Bunge za ukaguzi wa hesabu Kamati hizo zitawasilisha taarifa zao katika Bunge la Februari, 2019 ikiwa utaratibu wa kawaida wa ratiba za mikutano ya Bunge zitakuwa kama miaka iliyopita.

Hivyo, tumeanisha hoja zilizoibuliwa na CAG kama sehemu ya kwanza ya uwajibikaji na dhana ya uwazi ndio inanzia hapo. Ripoti hizo za CAG zimewekwa wazi kwa umma katika tovuti ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu.

Kwa kuwa Sekta ya Elimu nchini inaratibiwa na Wizara mbili za Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na OR-TAMISEMI, tumefanya uchambuzi wa Ripoti za CAG kwa Serikali kuu na Serikali za Mitaa tukiangazia sekta ya elimu kwa ujumla.

2.3 Hoja za uwajibikaji katika Ripoti za CAG kuhusu Sekta ya Elimu

2.3.1 Fedha za Ruzuku zilitolewa bila kuzingatia uhalisia wa idadi ya wanafunzi.

Kwa mujibu wa CAG kwenye ripoti yake ya Hesabu za Serikali za Mitaa, alibaini kuwa kwa mwaka wa fedha 2016/2017, fedha zilizopelekwa kwenye shule za Msingi na Sekondari katika Serikali za Mitaa 28 (Halmashauri) kiasi cha shilingi bilioni 1.93 zilikuwa zimepungua.

Kwa maoni yetu sisi katika uchambuzi huu tunaona kuwa suala hili linaweza kumaanisha kuwa wanafunzi ambao wengi wao ni vijana katika shule za msingi na Sekondari waliathiriwa na upungufu huo wa fedha za ruzuku.

2.3.2 Kutotengwa fedha za kufuatilia utekelezaji wa Sera ya Elimu bila malipo

Katika ripoti yake, CAG kwa mwaka wa fedha 2016/17 CAG alibaini kuwa Serikali haikutenga fedha kufuatilia utekelezaji wa sera ya elimu bila malipo. Jambo hili kwa mujibu wa uchambuzi huu linaweza kuathiri utekelezaji na kupelekea matumizi yasiyo ya msingi endapo ufuatiliaji hautafanyika kabla ya ukaguzi wa hesabu.

2.3.3 Upungufu wa Miundombinu katika Shule za Msingi na Sekondari

CAG katika ripoti yake ya ukaguzi wa Serikali za mitaa mwaka 2016/17 alibaini kuwa kuna upungufu wa miundombinu katika sekta ya elimu hasa katika shule za Msingi na Sekondari katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 31. Upungufu ulionekana kwenye miundombinu inayojumuisha madarasa, maabara, vyoo, migahawa, nyumba za watumishi na viwanja vya michezo kwa asilimia 199 katika shule za Msingi na 375 katika shule za sekondari. CAG alibaini kuwa upungufu huo unaathiri wastani wa mwalimu mmoja kwa wanafunzi 45 (1:45) na pia idadi kubwa ya walimu imeshindwa kufika katika vituo vipya vya kazi hasa maeneo ya vijijini.

Hii maana yake ni kuwa wanafunzi ambao wengi wao ni vijana katika shule za msingi na Sekondari walikosa elimu bora inayochangizwa na uwepo wa miundombinu toshelevu. Tulipochambua hotuba ya bajeti ya OR-TAMISEMI kwa kwa mwaka wa fedha 2018/2019 tulibaini kuwa kuna ongezeko la miondombinu; japokuwa takwimu za ongezeko katika hotuba ile hazioneshi kuwa mahitaji halisi ya vyumba kwa elimu ya msingi na Sekondari ni kiasi gani.

Kwa mfano; hotuba ya OR-TAMISEMI (2018/19) bila kutaja mahitaji ni kiasi gani kwa elimu ya Sekondari, iliishia tu kusema kuwa vyumba vya madarasa viliongezeka kutoka 39,490 katika mwaka wa fedha 2016/2017 hadi vyumba 40,278 kufikia Februari, 2018 sawa na ongezeko la vyumba 788. Pia katika vyumba vya madarasa ya elimu ya msingi vyumba vya madarasa vimetajwa kuongezeka bila kubainisha mahitaji halisi ni kiasi gani! Kwa maoni yetu, endapo mahitaji halisi hayatajwi wala kubainishwa tunashindwa kubaini endapo ongezeko la miundombinu inayotajwa na Serikali, inaleta maana au haileti maana (significant change or not). Kwa hiyo, vijana wanaume kwa wanawake wanaopata elimu katika maeneo ya vijijini wanaweza kuendelea kukosa miundombinu ya kujifunzia hivyo kuzorotesha ubora wa elimu.

2.3.4 Kutokatwa Marejesho ya Bodi ya Mikopo

Tulipochambua ripoti ya CAG (2016/17), ilibainika kuwa kiasi cha shilingi milioni 81.8 hazikukatwa na Wakala wa Nyumba na Utafiti bila kuzirejesha Bodi ya Mikopo ya wanafunzi wa Elimu ya Juu. Kwa mujibu wa CAG, suala hilo ni kinyume cha sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu kifungu Kifungu Na. 20 (1) na (2). CAG pia alibaini kuwa Wakala wa Maabara za Serikali alikata makato ya milioni 97.7 lakini aliziwasilisha kwenye Bodi ya Mikopo kwa kuchelewa.

Suala hili linamaanisha kuwa ucheleweshaji na kutokatwa kwa fedha hizo kutoka kwa taasisi na wakala wa Serikali, ni kiashiria kuwa vijana ambao ni wanafunzi katika vyuo vya Elimu ya Juu wanaopaswa kupata haki ya mikopo wanaweza kukosesha haki hiyo kutokana na kutowajibika kwa wakala na taasisi husika katika makato na marejesho ya fedha za mikopo.

2.3.5 Miradi ya ujenzi iliyochelewa kukamilika.

Kwa mujibu wa Ripoti ya CAG ya Serikali Kuu mwaka 2016/17 illibaini kuwa Fungu 46 la wizara ya Elimu, Sayansi na Ufundi haikufanya ujenzi katika chuo cha Ualimu Ndala wenye gharama ya sh. 4,634,441,632.10. Ijapokuwa eneo la ujenzi lilikabidhiwa kwa mkandarasi mnamo tarehe 27.11.2017 na kuanza ujenzi tarehe 24.2.2018 kwa mujibu wa hotuba ya waziri wa Wizara Ya Elimu, Sayansi Na Teknolojia mwaka 2018/19.

Hii inamaana kuwa vijana ambao ni wanaufaika wakuu wa elimu wanakosa mazingira mazuri ya kujifunzia kwa wakati kutokana na ucheleweshwaji wa ujenzi wa miundombinu.

2.4 Hoja za uwajibikaji katika Ripoti ya CAG kuhusu sekta ya Afya

2.4.1 Ongezeko la Madeni ya Matibabu Nje ya Nchi Bilioni 45.7

Tulipokuwa tunachambua ripoti ya CAG ya ukaguzi wa hesabu za Serikali kuu katika Wizara ya Afya, alibaini kuwa kati ya mwaka 2011 na 30 Juni, 2017 wagonjwa 3,906 walipewa rufaa nje ya nchi na wengi wao wakitibiwa nchini India. Taarifa aliyopewa CAG na Balizi wa Tanzania nchini India ilionesha kuwa deni limeongezeka kutoka Bilioni 28.6 mpaka shilingi Bilioni 45.7 kati ya tarehe 1 Julai, 2017 na Desemba 2017.

Katika hali isiyokuwa ya kawaida, hili ni ongezeko kubwa ndani ya kipindi kifupi. CAG alisisitiza kuwa mbali na kuhatarisha usitishaji wa huduma ya matibabu nje ya nchi lakini pia alishauri kuwepo na mkakati wa kina wa kujenga uwezo wa ndani wa rasilimali watu na miundombini ya matibabu ili kupunguza matumizi makubwa ya fedha za kigeni nje ya nchi.

2.4.2 Miradi iliyopokea fedha lakini haikutekelezwa

CAG alibaini uwepo wa miradi iliyopelekewa fedha za umma jumla ya shilingi bilioni 7.79 kwa ajili ya miradi ya sekta mbalimbali ikiwemo sekta ya afya lakini haikutekelezwa katika halmashauri 19; kati ya Halmashauri hizo, Halmashauri ya Wilaya ya Moshi ilipelekewa shilingi milioni 35 ili kuongeza hadhi ya Zahanati ya Okaoni lakini mradi haukutekelezwa.

Katika uchambuzi huu, tuliona kuwa kutotekelezwa kwa mradi huo kungeweza kuwaahitiri vijana na wakazi wengine wa eneo hilo. Kama mradi huu ungetekelezwa na zahanati hiyo kuwa hospitali, huduma zote zingeweza kupatikana hapo hivyo kuhakikisha usalama wa afya za vijana waweze kufanya shughuli zao vyema.

2.4.3 Miradi iliyokamilika lakini haitumiki

Tulipochambua ripoti ya CAG ya Serikali za Mitaa (2016/2017) tuliona CAG ameibaini kuwepo kwa miradi miwili ya sekta ya afya ambayo ilikamilika lakini haikuwa inatumika kama ilivyokusudiwa. Miradi yenyewe ni pamoja na mradi wa ujenzi ulioghharimu milioni 83.2 na haukuwa unatumika katika Halmashauri ya Wilaya ya Babati ujenzi wa zahanati 3 za Gesbert, Boay, Sabiro na Kituo cha afya cha Ufana

Pia mwaka 2015 miradi ya ujenzi ulioghharimu shilingi milioni 21.3 wa chumba cha kuhifadhi maiti ilikamilika lakini haikuwa inatumika katika halmashauri ya wilaya ya Moshi ni pamoja na chumba cha maiti katika kituo cha Afya Shimbwe, na ujenzi wa vyumba vya maabara awamu ya tatu.

Kutokana na uchambuzi huu, kutotumika kwa miradi hii inaweza kuchangia katika ongezeko la uhaba wa ajira kwa vijana wanaohitimu mafunzo yao ya afya. Vituo hivi vya afya vingeweza kuajiri vijana wengi na kupunguza idadi ya vijana wasio na ajira nchini.

2.4.4 Fedha za Sekta ya Afya milioni 475.5 ambazo huenda hazikufika kunakostahili

Wakati kikosi kazi kinafanya uchambuzi wa Ripoti ya CAG ya Serikali za Mitaa (2016/2017) iliona kuwa CAG amebaini tofauti ambayo haikusuluhishwa (bank reconciliation) ya shilingi milioni 475.5. Barua ya salio kutoka OR-TAMISEMI kwenda kwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa ilionesha kuwa kiasi cha shilingi Bilioni 3.9 zimepelekwa kwenye sekta ya Afya ila kiasi kilichokutwa Benki kuu na CAG ni shilingi Bilioni 3.4 hivyo kupelekea tofauti ya shilingi milioni 475.5

CAG (2016/17) katika sekta ya afya kwenye ripoti yake pia alibaini uwepo wa masula ya kihakababu katika ukosefu wa taarifa ya usuluhishi wa kibenki kwenye mapato ambayo endapo maelezo hayawezi kupatikana basi mambo hayo yanaweza kuzua mashaka. Mfano CAG alibaini; Mapato kwenye taarifa za Benki lakini hayapo kwenye daftari la fedha shilingi 24,982,934,155.53, Malipo kwenye taarifa za Benki lakini hayapo kwenye daftari la fedha Shilingi (3,952,144,431), Mapato kwenye daftari la fedha lakini hayapo kwenye taarifa za Benki (SH.TZ) 25,890,229,470 na malipo kwenye daftari la fedha lakini hayapo kwenye taarifa za Benki shilingi (837,041,194)

2.4.5 Miradi ya Maendeleo Sekta ya Afya iliyopewa fedha pungufu

Tulipochambua ripoti ya CAG ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa, (2016/17) tuliona kuwa imebainika kuwa ipo miradi yenye thamani ya shilingi bilioni 1.05 ambayo haikutekelezwa kwenye sekta mbalimbali ikiwepo sekta ya afya katika Halmashauri ya Jiji la Mwanza. Miradi ambayo haikutekelezwa kutokana na kupokea fedha pungufu ni pamoja na kumalizia ujenzi wa kituo cha afya cha Bullae pamoja na kumalizia ujenzi wa kituo cha afya cha Isabenda. Kwa maoni yetu, kupeleka fedha pungufu katika kumalizia kituo cha afya cha Bullae na Isabenda kunaweza kuathiri huduma za mama na mtoto, kuathiri kundi rika la vijana wanaume kwa wanawake.

3.0 HALI YA RUSHWA KATIKA SEKTA ZA ELIMU NA AFYA

3.1 Maana ya Rushwa na Msingi wa Uchambuzi

Kundi kubwa la wanaojihusisha na masuala ya rushwa nchini Tanzania kwa zaidi ya asilimia 60 ni kati ya umri wa miaka 25 na 44, huku umri kati ya miaka 25-34 wakiwa asilimia 33(EABI,2017). Mpaka mwaka 2017, Tanzania katika takwimu za ulimwengu Tanzania ilishikilia rekodi ya kuwa nchi 103 kati ya nchi 180 kwa kiwango cha rushwa, (CPI Index, Transparency International, 2017).

Rushwa haina tafsiri moja, benki ya dunia kwa mfano, inatafasiri rushwa kama kitendo cha matumizi mabaya ya ofisi ya umma au ofisi ya shirika binafsi ili kujipatia faida binafsi isivyohalali. Zipo aina mbalimbali za rushwa katika mifumo ya utawala. Benki ya dunia imetaja takribani aina sita za rushwa.

Rushwa kubwa (Grand Corruption); ambayo inahusisha wakuu wa nchi na Serikali, mawaziri, makatibu wakuu wa wizara, wakurugenzi waandamizi wa mashirika ya umma, wanasiasa na kuhusisha wafanyabiashara wakubwa katika kujipatia faida binafsi.

Rushwa aina ya pili ni rushwa ya kisiasa (Political corruption) inayowahusisha watunga sheria kama vile wafalme, viongozi wa kiimla (madikteta) ambao hujichukulia uamuzi wa kutunga sheria na kanuni zinazowanufaisha wao binafsi kwa kisingizio cha kutumikia umma.

Aina ya tatu ya rushwa ni rushwa ya makampuni (Corporate Corruption) ambayo huhusisha makampuni ya kibiashara baina yao kwa upande moja na wateja wao au wazabuni wao kwa upande mwingine ili kujipatia manufaa kibiashara.

Rushwa aina ya nne ni rushwa ya kiutawala (administrative corruption) ambayo inahusisha hongo na upendeleo katika watu au wafanyabiashara katika kujipatia nafasi kazini, kupunguziwa kiwango cha kodi na tozo, kukwepa kanuni, sheria ili kujipatia mikataba ya zabuni kwenye manunuzi.

Aina ya tano ya rushwa ni rushwa ndogo (Petty corruption) ambayo ni hongo inayotolewa na mtu wa kawaida ili kurahisisha utoaji wa huduma katika sekta mbalimbali za utoaji wa huduma za umma.

Rushwa aina ya sita iliyobainishwa na Benki ya Dunia ni rushwa ya kimfumo (systematic corruption), hii ni aina ya rushwa inayotawala mifumo mbalimbali ya maisha ya kijamii.

Kwa upande wake, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini, (PCCB) kutokana na utafiti wake wa mwaka 2017 ilihitimisha kuwa kiwango kikuu cha rushwa kilichobainishwa na wananchi pamoja na wafanyabiashara ni kitendo cha kudai hongo yaani malipo ya fedha yasiyo ya kiofisi hivyo kuifanya rushwa ya aina hii kuitwa rushwa ndogo yaani (petty corruption).

Hivyo basi, katika uchambuzi huu, tumepitia ripoti tatu tofauti ili tuweze kubaini hali halisi ya rushwa ndogo (Petty corruption) katika sekta za Elimu na Afya. Tumechambua ripoti zilizotolewa hivi karibuni ikiwepo ripoti ya Afrika Mashariki kuhusu Viashiria vya rushwa (East Africa Bribery Index, 2017) iliyochapishwa na shirika la Transparency International. Tumechambua ripoti ya rushwa ya Afrobarometer, 2017 na pia tumechambua ripoti ya rushwa ya Shirika la Tanzania la Kuzuia na Kupambana na Rushwa (PCCB) ya mwaka 2017.

Ufuatao ni uchambuzi wa hali ya rushwa katika sekta za elimu na afya ambao unazingatia namna vijana wanavyoathiriwa na uwepo wa rushwa hizo katika muktadha mpana wa utoaji wa huduma za elimu na afya kwa kuzingatia uwiano wa kijinsia.

3.2 Kiwango cha Rushwa ndani ya sekta ya Elimu

Watu wengi hutoa hongo kwa lengo la kuharakisha utoaji wa huduma. Hivyo maboresho yoyote ya utoaji wa huduma kwa umma zinazingatia uwiano wa kijinsia, unaweza kupunguza hongo kwa kiwango kiubwa. Ilibainika kuwa asilimia 37 ya wanaotoa hongo hufanya hivyo ili kurahisisha upatikanaji wa huduma (EABI, 2017). Sekta ya elimu nchini Tanzania inatoa huduma kadhaa kupitia mashirika ya umma, shule na vyuo vya elimu ya ufundi na elimu ya juu.

Kiwango cha rushwa katika taasisi za elimu nchini Tanzania kimebainika kuongozeka kutoka asilimia 12.2 mwaka 2014 mpaka kufikia asilimia 14.2 mwaka 2017 (EABI, 2017); hata hivyo kitaifa kwa mujibu wa Ripoti ya Viashiria vya Rushwa Afrika Mashariki (East Africa Bribery Index, 2017) ukiangalia mgawanyo wa hongo kitaifa (share of bribery paid), sekta ya elimu ilishika nafasi ya tano kwa asilimia 8.4 mwaka 2017 ikishuka kwa asilimia 1 kutoka asilimia 9.1 iliyorekodiwa mwaka 2014 wakati Sekta ya Jeshi la Polisi ikiongoza kwa kushika nafasi ya kwanza kwa asilimia 32 mwaka 2017 na asilimia 25.6 mwaka 2014.

Wakati huo huo, utafiti wa PCCB kwa mwaka huo huo wa 2017 ukionesha kuwa kwa kiwango kikubwa cha asilimia 41.1 huku kiwango kidogo kikirekodiwa katika asilimia 20.3; na kinara wa hongo ikibakia kuwa Jeshi la Polisi lililokuwa na kiwango kikubwa cha rushwa kwa asilimia 83.5, Trafiki wakiwa asilimia 85.3.

Hata hivyo, sehemu kubwa ya Watanzania hawaripoti matukio ya rushwa wakiamini kuwa hata wakitoa ripoti hakuna hatua zozote zitakazochukuliwa. Takribani watu 8 kati ya 10 mwaka 2017 hawakuripoti kuhusu matukio ya hongo (EABI, 2017), Tulipopitia ripoti mbalimbali za Rushwa ilibainika kuwa wananchi wanadhani kuwa kiwango cha rushwa kwa ujumla kimepungua kwa asilimia 70 (EABI, 2017) wakati ripoti ya Afrobarometer ikionesha kuwa kiwango cha rushwa kimepungua kwa asilimia 72. Wakati huo huo asilimia 74 wakisema kuwa wanadhani Serikali inawajibika kupambana na rushwa na asilimia 20 wakisema kuwa wao wanaona Serikali haitimizi wajibu wake. (EABI, 2017). Kati ya sababu tano za kudhani kuwa Serikali inawajibika kupambana na rushwa, zilitajwa utumbuaji wa watumishi wa umma (23%), kupungua kwa kiwango cha hongo (18%), juhudi za serikali kuzima rushwa (16%), kuanzishwa mahakama ya mafisadi (13%), na juhudi za Rais kupinga rushwa (9%), sababu nyinginezo (19%).

Kutokana na uchambuzi huu tulioufanya inaonesha wazi vijana ni waathirika wakubwa wa vitendo vya rushwa katika sekta ya elimu nchini ikiwemo rushwa ya ngono kwa wanafunzi wakike.

3.3 Kiwango cha rushwa ndani ya sekta ya afya.

Kwa mujibu wa Shirika la Kudhibiti na Kupambana na Rushwa nchini (PCCB) katika utafiti wao kuhusu rushwa uliofanywa mwaka 2017 kati ya matatizo sugu matano yanayowakabili Watanzania, huduma duni za afya ilishika nafasi ya nne. Utafiti huo uliwataka wananchi waseme wanadhani kwa maoni yao yepi ni matatizo yanayowakabili Watanzania, utafiti ulibainisha kuwa tatizo la kwanza ni *mfumuko wa bei* (12.7%) ikifuatiwa na *gharama kubwa za maisha* (12.4), *Ukosefu wa ajira* (11.1%), *huduma duni za afya* (10.8%) na mwisho *huduma duni za elimu* (8.5). Kwa mujibu wa PCCB inaaminika kuwa matatizo hayo ndio kichocheo kikubwa cha uwepo wa rushwa. Inakadiriwa kwa kiwango cha asilimia 47 unaweza kukumbana na kadhia ya kuombwa hongo ukienda kupata huduma kwenye taasisi za Afya nchini Tanzania. (EABI, 2017).

Katika utafiti huo huo wa (PCCB, 2017) ilibainika kuwa asilimia 67.4 ya wananchi waliohojiwa walidai kuwa taasisi za sekta ya afya zinajihusisha na vitendo vya rushwa kwa kiasi kubwa mno, huku asilimia 17.6 wakisema wanadhani kiwango cha rushwa ni cha wastani katika taasisi hizo za afya.

Katia utafiti uliofanywa na shirika la Vijana Restless Development kwa kushirikiana na asasi nyigine za vijana ikiwemo TYVA mwaka 2015, utafiti ule ulibaini kuwa “vijana wa 3 tu kati ya 10 wanakubali kuwa rushwa na urasimu (mlolongo), umedhibitiwa katika kupata huduma ya afya. Hii inamaanisha kuwa vijana wenyewe bado wanaamini kuwa rushwa kwenye sekta ya afya ni tatizo sugu.

Kiwango cha rushwa kimeongezeka katika taasisi za huduma za afya nchini Tanzania kutoka asilimia 15.2 mwaka 2014 mpaka kufikia asilimia 20.7 mwaka 2017 (EABI, 2017). Kitaifa kwa mujibu wa Ripoti ya Viashiria vya Rushwa Afrika Mashariki (East Africa Bribery Index, 2017) ukiangalia mgawanyo wa hongo kitaifa (share of bribery paid), sekta ya afya ilishika nafasi ya tatu kwa asilimia 11.3 mwaka 2017 ikishuka kwa asilimia 2 kutoka asilimia 9.2 iliyorekodiwa mwaka 2014 huku Sekta ya Jeshi la Polisi ikiongoza kwa kushika nafasi ya kwanza kwa asilimia 32 mwaka 2017 na asilimia 25.6 mwaka 2014.

Kwa upande mwingine ripoti ya Afrobarometer inaonesha kuwa kiwango cha vitendo vya rushwa kwa mwaka 2014 ilikuwa asilimia 67 huku kwa mwaka 2017 ikishuka hadi asilimia 10. Huku ripoti hii ikiweka wazi kuwa kwa mwaka 2014 nguvu ya serikali kupambana na vitendo vya rushwa ilikuwa asilimia 37 tu na kwa mwaka 2017 serikali imeonekana ikiongeza nguvu ya kupambana na vitendo rushwa kwa asilimia 71.

Aidha imebainika kupitia ripoti ya Afrobarometer kuwa kwa mwaka 2017 asilimia 24 ya watu walio hojiwa na wanaojua taasisi ya kupambana na kuzuia rushwa PCCB walidai kuwa taasisi hiyo kuwa inapambana na rushwa kwa nguvu kubwa mno na juhudi haswa, na kwa upande mwingine asilimia 59 walidai kuwa taasisi hiyo inapambana na vitendo vya rushwa kwa kiwango cha kawaida tu.

4.0 HITIMISHO

Kupitia uchambuzi huu, TYVA inataka kuwaleta pamoja vijana kupitia taasisi zao katika mjadala wenye lengo la kuibua mikakati mbalimbali ya kupambana kwa pamoja dhidi ya matumizi mabaya ya rasilimali za umma na kupambana dhidi ya rushwa. Katika hatua hii, TYVA inatumia uchambuzi huu kuibua mjadala mpana unaojikita kwenye sekta za elimu na afya katika uwajibikaji, Uwazi na mapambano dhidi ya rushwa.

Hivyo basi, mjadala baada ya uchambuzi huu utajikita kwenye hoja za sekta ya elimu na afya zilizoibuliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) katika ripoti zake za Jumla kuhusu Hesabu za Serikali Kuu na Hesabu za Mamlaka ya Serikali za Mitaa (2016/17); Lakini pia mjadala utaangalia kwa kina hali ya rushwa kwenye sekta hizo mbili za elimu na afya.

Kwa mfano hoja za sekta ya elimu zilizoibuliwa katika uchambuzi huu ambazo zitajadiliwa kwa kina na kuwekewa mkakati wa ushawishi na utetezi ni pamoja na *uwepo wa fedha za Ruzuku zilitolewa bila kuzingatia uhalisia wa idadi ya wanafunzi, kutotengwa fedha za kufuatilia utekelezaji wa Sera ya Elimu bila malipo, upungufu wa Miundombinu katika Shule za Msingi na Sekondari, kutokatwa marejesho ya bodi ya mikopo na Miradi ya ujenzi iliyochelewa kukamilika*. Katika sekta ya afya, vijana watabuni mikakati ya ushawishi na utetezi kuhusu hoja ambazo ni pamoja na *ongezeko la madeni ya matibabu nje ya nchi bilioni 45.7, miradi iliyopokea fedha lakini haikutetelezwa, miradi iliyokamilika lakini haitumiki, fedha za sekta ya afya milioni 475.5 ambazo huenda hazikufika kunakostahili na miradi ya maendeleo sekta ya afya iliyopewa fedha pungufu*

Kwenye mikakati ya kupambana na rushwa, vijana watajadili namna ya kuboresha huduma za afya na elimu zinazozingatia uwiano wa jinsia kama moja ya mbinu ya kudhibiti rushwa. Kwa kuwa ilibainika kuwa wengi wa watu hutoa hongo ili kuchochea kupatikana kwa huduma. Pia uchambuzi ulibaini shida zinazowakabili wataanzania zina uhusiano wa moja kwa moja na kiwango cha rushwa. Shida hizo ni pamoja na mfumuko wa bei, kubwa za maisha, Ukosefu wa ajira, huduma duni za afya na mwisho huduma duni za elimu. Viashiria hivi vya shida za wananchi vilivyobainishwa kwenye sekta za elimu na afya ndivyo ambavyo mjadala utajielekeza huko ili kuviundia suluhisho hasa kuhusu mtazamo wa Watanzania juu ya rushwa.

Ni matokeo ya mjadala huo wa vijana utakaopendekeza hatua ambazo vijana wanadhani ni muhimu zikachukuliwa baina ya wadau mbalimbali wanohusika katika mapambano dhidi ya rushwa, uwajibikaji na Uwazi katika sekta zinazoangaliwa. Vijana wa TYVA wanatazamia kuwa mikakati itakayoibuliwa katika mjadala huo utapelekea kufanyika kwa shughuli za ushawishi na utetezi wenye lengo la kuongeza tija katika utoaji wa huduma za elimu na afya unaozingatia uwiano wa kijinsia.

5.0 REJEA

Restless Development (2015). *Hali ya vijana Tanzania*, Dar es Salaam

TI (2017). *East Africa Bribery Index*, Nairobi, Kenya

PCCB (2017) *Mini-Baseline Survey Report Based On The Developed National Corruption And Ant-Corruption Effort Indicators*, URT, Dar es Salaam

World Bank (2005). *The Cancer of Corruption*,

TI (2017), *Corruption Perception Index 2017*,

URT (2018). *Budget Speech 2018/19, Ministry of Health, Community Development, Gender, Elderly and Children*. Dodoma

URT (2018). *Budget Speech 2018/19, President's Office Regional Administration and Local Government*, Dodoma

URT (2018). *Budget Speech 2018/19, the Ministry of Education, Science and Technology*, Dodoma

Afrobarometer (2017) *In Tanzania, anti-corruption efforts seen as paying dividends need citizen engagement*

URT (2007) *National Health Policy*. Dar es Salaam. Government Publisher

URT (2007) *Education and Training Policy*. Dar es Salaam. Government Publisher

CAG, (2018) [Central Government General Audit report 2016/17](#)

CAG, (2018) [Local Government General Audit Report 2016-17](#)

Antonio Andreoni (2017) *Anti-Corruption in Tanzania: A political settlements analysis*